

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI  
JESHI LA POLISI TANZANIA**

Anuani ya Simu "MKUUPOLISI"  
Simu: (026) 2323585  
Fax Na: (026) 2323586



Ofisi ya Mkuu wa Jeshi la Polisi,  
Makao Makuu ya Polisi,  
4 Mtaa wa Posta,  
S.L.P 961,  
40483 DODOMA.

**19/01/2022**

**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI**

**Ndugu wanahabari,**

Jeshi la Polisi lingependa kupitia kwenu, kuwajulisha wananchi kuwa hivi karibuni litaanza kutumia mashine mpya ya kijiditali za kulipia tozo mbalimbali ambazo zimenunuliwa kwa fedha zilizotolewa na serikali ili kutatua chanagamoto na malalamiko yaliyokuwa yanatolewa na wananchi.

**Ndugu wanahabari,**

Kama mnavyokumbuka serikali ilishotoa maelekezo ukusanyaji wa maduhuri au ulipiaji wa tozo mbalimbali ufanyike kwa njia ya kielekroniki. Lakini pia mtakumbuka kulikuwepo na malalamiko kutoka kwa madereva wa vyombo vya moto kuwa walikuwa wakibambikiziwa faini ya makosa ya usalama barabarani ambayo hawakutenda au kwa siku wanayoambiwa walitenda kosa hawakuwepo katika eneo hilo hata gari anayoendesha haikufika eneo hilo.

Aidha malalamiko mengine yaliyokuwa yakitolewa na madereva ni kwamba namba ya gari iliyoandikwa katika risiti ya faini ni gari analoendesha lakini namba ya leseni ya udereva sio ya kwake

**Ndugu wanahabari,**

Jeshi la Polisi lingependa kueleza kuwa changamoto na malalamiko yanakwenda kutatuliwa na mashine hizi mpya kutokana na uwezo wake

kijiditali wa kuweza kuchukua kumbukumbu mbalimbali, zitakazo tatua changamoto hizo.

Mashine hiyo ambayo itazinduliwa hivi karibuni inajulikana kwa jina la Android Poss Machine ambayo ina uwezo wa kuchukua taarifa na kumbukumbu kama inavyofanya simu janja (Smartphone) kwa ajili ya matumizi mbalimbali.

Mashine hizi ( Android Poss Machine) zina uwezo wa kufanya yafuatayo:

1. Ina kioo kwa mbele kinachoruhusu kuingiza kumbukumbu tofauti na zile za awali zilizokuwa na vibonyezo (Button).
2. Ina uwezo wa kuchukua alama za vidole hivyo ikitokea dereva anaandikiwa faini atachukuliwa pia alama ya vidole na mashine hiyo.
3. Mashine hii inaweza kupiga picha leseni na namba ya gari kwani ina kamera (Ina uwezo wa ku-scan nyaraka).
4. Pia inao uwezo wa kuhifadhi kumbukumbu kwa ajili ya rejea ya baadaye.
5. Itakuwa na orodha yote ya makosa 37 ya usalama barabarani.
6. Itatumika katika kulipia maduhuli mbalimbali ya serikali kama vile loss report, kulipia silaha, ukaguzi wa gari (Vehicle Inspection report).
7. Inauwezo wa kutumika katika eneo lolote kwani inaweza kutumia mtandao wa kampuni ya simu zaidi ya moja na pia kutumia wifi. Kasi yake ya mtandao (internet) ni ya 4G tofauti na poss ya awali iliyokuwa na spidi ya 2G.
8. Itakuwa na uwezo wa kusoma taarifa za TRA kama vile kulinganisha kumbukumbu za leseni ya udereva au namba ya gari na jina la mmiliki

## **Ndugu wanahabari**

Katika maandalizi ya kuanza kutumia mashine hizi kinachoendelea hivi sasa ni pamoja na kutoa elimu kwa wananchi kupitia vyombo vya habari ambayo inatolewa na wataalamu wa kitengo cha Tehama cha Polisi na kikosi cha usalama barabarani.

## **Aksanteni kwa kunisikiliza**

### **Imetolewa na:**

David A. Misime - SACP

### **Msemaji wa Jeshi la Polisi**

Makao Makuu ya Polisi

Dodoma, Tanzania

[www.polisi.go.tz](http://www.polisi.go.tz)

[www.twitter.com/tanpol](https://www.twitter.com/tanpol)

[www.facebook.com/tanpol](https://www.facebook.com/tanpol)

[www.instagram.com/polisi.tanzania](https://www.instagram.com/polisi.tanzania)